HOTUBA YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA KAGERA MEJA JENERALI (MST) SALUM MUSTAFA KIJUU WAKATI WA UZINDUZI WA MRADI WA KUREJESHA HALI ZA WANANCHI WALIOATHIRIKA NA TETEMEKO LA ARDHI MKOANI KAGERA KUPITIA SEKTA ZA KILIMO NA MIFUGO TAREHE 5 MEI, 2017 KATIKA UKIMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA WA KAGERA.

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,
Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba,
Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,
Ndugu Mwakilishi wa FAO Tanzania,
Ndugu Mwakilishi Ofisi ya Rais TAMISEMI,
Ndugu Mwakilishi Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi,
Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wa Serikali,
Ndugu wa Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali,
Ndugu Wana Habari Mliopo hapa,
Mabibi na Mabwana,

Habarini za asubuhi:

Ndugu washiriki: Kwanza kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kagera napenda kuchukuwa fursa hii kulishukuru shirika la kilimo na chakula duniani (FAO) kwa kuguswa na matatizo ya

Tetemeko la Ardhi pamoja na ukame yaliyotupata mwishoni mwa mwaka jana.

Ndugu washiriki: Matatizo yaliyotupata yalisababisha madhara makubwa sana si kwa wananchi tu wa Mkoa wa Kagera lakini pia hata kwa Serikali. Wananchi wengi walioathirika na tetemeko la ardhi ni wale wa kiapato cha chini ambao kwakweli uwezo wao wa kurejesha hali na maisha yao ya awali ni mdogo sana na hivyo kusababisha wananchi hao kuwa na maisha duni.

Ndugu washiriki: Mbali na tetemeko la ardhi, Mkoa wetu pia ulipitia katika kipindi kigumu cha ukame katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilipelekea mazao mengi yaliyokuwa mashambani kukakuka jambo ambalo lilipelekea kuwa na upungufu wa chakula kwa baadhi ya maeneo.

Ndugu washiriki: Serikali kwa upande mmoja imefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa wananchi wa Mkoa wa kagera wanarejea katika hali yao ya awali kabla ya matatizo hayo mawili niliyoyataja hapo juu**.** Serikali imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali wenye nia njema na Mkoa wa Kagera kusaidia katika kurejesha hali za wananchi wetu kwa namana mbalimbali.

Ndugu washiriki: Napenda kutamka wazi kuwa Shirika la Kilimo na Chakula duniani (FAO) ni miongoni mwa wadau wachache ambao wameguswa kwa namna ya tofauti kwa

kuamua si tu kutoa msaada wa vitu lakini wameamua kufanya jambo ambalo kama likisimamiwa vizuri litakwenda kuacha alama katika Mkoa wetu wa Kagera kwani wametekeleza ile kauli ya kwamba "Usimpe mtu samaki bali mpe nyavu na kumfundisha namna ya kuvua samaki".

Ndugu washiriki: Mwanzoni mwa mwezi januari, 2017 Ofisi yangu kupitia Katibu Tawala Mkoa ili andika barua kwa Mwakilishi wa Shirika la Kilimo na Chakula duniani (FAO) kwa lengo la kuomba msaada wa mbegu za mazao yanayotumia maji kwa ufanisi ili kuwasaidia wananchi wetu mbegu za kupanda wakati mvua zitakapoanza kunyesha.

Ndugu washiriki: Wakati mwingine kutokana na mzigo tuliokuwa nao wa kuwasaidia wananchi wetu, tuliona kuwa barua ya maombi yetu inachelewa kujibiwa**.** Hata hivyo Nilitoa maagizo kwa Halamshauri zote kuhakikisha zinatenga fedha ya kununua mbegu japo kidogo na pia kuhamasisha wananchi kulima mazao yanayotumia maji kwa ufanisi. Jambo ambalo limetekelezwa na Halmashauri zote.

Ndugu washiriki: Waswahili husema "*kimya kingi kina mshindo"*. Hili limejidhihilisha wazi hii leo ambapo tunazindua Mradi mkubwa kwa Ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ambao si tu kwamba utasaidia upatikanaji wa mbegu lakini pia utajikita kutoa mafunzo ya kilimo pamoja na ufugaji kwa wakulima na wafugaji katika Halmashauri zilizomo kwenye Mradi.Pia

Mradi utatoa mafunzo mbalimbali ya kukabiliana na majanga mbalimbali yakiwemo matetemeko ya ardhi na ukame kabla na hata baada ya kutokea. ***NASEMA ASANTENI SANA*.**

Ndugu washiriki: Mradi huu utatekelezwa katika Halamshauri tano (Muleba, Kyerwa Bukoba Dc, Missenyi na Bukoba Manispaa) za Mkoa wa Kagera na kwamba jumla ya kaya 5,000 zinatarajiwa kunufaika moja kwa moja na mradi huu. Idadi hii si haba, Hata hivyo Nina imani kwamba kadri mradi utakavyokuwa unaendelea, Shirika la Kilimo na Chakula duniani (FAO) litaangalia uwezekano wa kutanua wigo wa mradi ili uweze kuzifikia na Halmashauri zingine tatu zilizobaki (Ngara, Biharamulo na Karagwe) kwa kadri watakavyoona inawezekana.

Ndugu washiriki: Nina matarajio makubwa sana na mradi huu ambao ninauzindua siku ya leo kwamba utakwenda kuleta matokeo mazuri na makubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera hususani Halmashauri ambazo zipo katika mradi.

- **Kwanza,** Nitoe wito kwa Watendaji na Watekelezaji wote wa mradi, Tumekuwa na miradi mingi sana katika sekta za Kilimo na Mifugo, Miradi ambayo imetekelezwa kwa gharama kubwa za Serikali na Wadau wa Maendeleo. Miradi hiyo pamoja na gharama kubwa zilizotumika haijaweza kuleta tija kwa kiwango kilichotegemewa.

- **Pili,** Nichukuwe fursa hii kuwaagiza Watendaji wote wa Halmashauri amabazo zimebahatika kuingia katika mradi huu "Hakikisheni kwamba Mnasimamia na kufuatilia kwa umakini mkubwa utekelezaji wa mradi huu." Hatuwezi kuwa kila wakati Serikali na Wadau wanatoa fedha kutekeleza miradi halafu hatuoni mabadiliko. "Hili sitalivumilia"

Ndugu washiriki: Leo ni siku ya uzinduzi, Kubwa ambalo napenda kuahidi hapa mbele ya Mwakilishi wa FAO Tanzania, ni kwamba " ***Mimi na timu yangu tutafuatilia kwa ukaribu mkubwa sana utekelezaji wa mradi huu kuanzia hatua ya mwanzo".***

Baada ya kusema hayo natamka rasmi kwamba Mradi huu wa kurejesha hali za wananchi walioathirika na tetemekola Ardhi na ukame Mkoani Kagera kupitia sekta za Kilimo na Mifugo, ***Nimeuzindua rasmi leo tarehe 05 Mei, 2017.***

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA